# GRADE 4 END OF YEAR EXAMS

# KISWAHILI

# Time: 1Hour

**Soma mazungumzo haya kisha ujibu maswali 1 hadi 5.**



**Halima**: Hamjambo wanangu?
**Wendy na Lucy**: ___1___ mama u hali gani?
**Halima:** Wendy nenda utayarishe meza ili tuandae kiamsha ___2___.
**Wendy:** Aya mama.
**Halima**: Lucy peleka chungu ___3___ kwa moto.
**Lucy**: Mama chungu kizito, sikiwezi.
**Halima**: Najua wewe ni ___4___ basi nenda ukasaidie dada ___5___ kuandaa meza.
**Lucy**: Sawa mama.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Sijambo | Hujambo | Hatujambo | Jambo |
| 2. | Kimya | Kinywa | Kinyua | Kunywa |
| 3. | hiki | hii | hili | huu |
| 4. | msembe | mzebe | mzembe | mizembe |
| 5. | lako | wako | zako | yako |

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 6 hadi 9.**

Kazungu ana tabia ya wizi. Siku moja alikata kauli kwenda katika sherehe za kuanzia mwaka. Aliandamana na watoto wenzake waliomcheka kwa sababu hakuwa na hata shilingi moja mfukoni ya matumizi madogo. Kazungu alikasirika sana. Alisukumana nao na kuwatisha wampe pesa walizo nazo.

Watoto hao waliogopa na kuanza kukimbia ovyo. Kazungu alifanikiwa kuiba pesa za sarafu pekee. Watoto hao walienda moja kwa moja hadi kituo cha polisi. Walimshtaki Kazungu. Uchunguzi ulipofanyika na ukweli wote kupatikana na Kazungu aliadhibiwa.